**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**

**SHULE YA SEKONDARI MUUNGANO-1**

**S.L.P 204**

TUNDUMA – SONGWE.

**25/11/2021**

MWANAFUNZI ..............................................................
S.L.P. ..........................................................................

**MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MUUNGANO-1 ILIOPO HALMASHAURI YA MJI WA TUNDUMA MKOA WA SONGWE KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2022**

**1.0 UTANGULIZI.**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka **2022** Shule ya sekondari **MUUNGANO -1** ipo Mjini Tunduma umbali wa KM 2 kutoka kituo kikuu cha mabasi kuelekea njia ya mkombozi. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **17/01/2022** . Zoezi la kusajili kidato cha kwanza litachukuwa siku mbili. Wahi siku hizo ili kuepuka usumbufu. **na kuchelewa masomo**

***UNATAKIWA KURIPOTI SHULENI TAREHE HIYO BILA KUKOSA. IWAPO KUNA TATIZO LENYE KUPELEKEA KUCHELEWA TOA TAARIFA. VINGINEVYO HATUPOKEI MWANAFUNZI ALIYE CHELEWA BILA TAARIFA.***

**2.0 MAMBO YA KUZINGATIA.**

**2.1 SARE YA SHULE**

(a) Sare ya shule hii ni kama ifuatavyo:-

**WAVULANA.**

- Mashati mawili meupe na yenye mikono mifupi.
- **Tai mbili ( kijivu -1, na kijani mpauko 1)**
- Suruali mbili **kijivu 1 na kijani mpauko 1**
  *Mifuko mitatu ya kawaida na siyo mshono wa jeans.
  *Suruali za kubana *kamwe* hazikubaliki hapa shuleni.
- **Sweta mbili za dark blue**
- Viatu vyeusi vyenye kamba jozi mbili na vyenye visigino vifupi na soksi nyeusi au blue jozi mbili.

**WASICHANA.**

- Mashati mawili meupe na yenye mikono mifupi.
- Sketi mbili **kijivu 1 na kijani mpauko 1 "mshono wa linda box"**
  *Mikunjo/Malinda madogo sana ama makubwa sana *kamwe* hayakubaliki, aidha sketi sharti iwe ndefu kufikia kifundo cha mguu.
- **Sweta mbili za dark blue**

- Viatu vyeusi vyenye kamba jozi mbili na vyenye visigino vifupi na soksi **nyeupe jozi mbili**

(b) Sare ya michezo (kwa wavulana na wasichana);

- Track suit rangi **ya kijivu** tepe nyeupe.
- Raba/"njumu" jozi **moja**
- Soksi ndefu rangi bluu.

## 2.2 VIFAA VYA DARASANI

- Daftari kubwa **tisa** - counter books (kuanzia 2-quire au Zaidi)
- Mkebe mmoja.
- Rula moja.
- Karamu za wino bluu au nyeusi pia za risasi za kutosha.
- File folder 1
- Picha 2 PPS
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- Vitabu vya masomo mbalimbali na kamusi ya kiingereza.

## 2.3 HUDUMA YA AFYA

- Shule ipo karibu sana na Kituo cha afya cha Serikali hivyo mzazi/mlezi unashauriwa kumkatia bima ya afya mwanao ili apate huduma bila vikwazo.
- **Mwanafunzi afike na Fyekeo, jembe na kindoo cha litakumi kwaajili ya usafi**

# 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

3.1 **Muungano-1** Sekondari inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu namba 25 ya 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi Na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa Viongozi, Wazazi/Walezi,Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu ***Utoro kamwe haukubaliki..***

(c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni/kazi unazopewa na walimu kuzifanya nyumbani

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo Ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(i) Kutunza mali za Umma na zako binafsi kwa makini.

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ***ukafukuzwa shule.***

1 .Wizi
2. Uasherati na Ushoga.
3.Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine, mirungi, kubeli n.k
5. Kupiga na kupigana.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa ama Wimbo wa Taifa.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au Watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
15. Kuwa na simu ya mkononi/ama kupatikana na simu ya mkononi.

**4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU;-**

(a) Uje na Taarifa ya afya (Medical examination) kutoka hospitali ya serikali.
(b) Uje na barua ya kuahidi kuto shiriki katika migomo, Fujo na makosa ya jinai.
(c) Uje na barua ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubariana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**5.0** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu ili kuepuka ***USUMBUFU USIO WA LAZIMA***.

*UJE UKIWA UNAJUA UNAKUJA SHULENI KUFANYA NINI. TUNAWAPENDA SANA NA KUWASAIDIA KWA MOYO WANAFUNZI WENYE NIA YA KUPATA ELIMU NA STADI ZA MAISHA ILI KUYAKABILI MAISHA YAO YA SASA NA BAADAYE.HAWA DAIMA NI WATII, WANAJUHUDI NA HUZINGATIA RATIBA NA TARATIBU ZA SHULE PASIPO SHURUTI. JITAHIDI UWE MIONGONI MWAO.

**Karibu sana Shule ya sekondari Muungano-1**

**YUSTER M. BONEPHACE**
MKUU WA SHULE

**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**

**SHULE YA SEKONDARI MUUNGANO-1**

**FOMU YA KUKUBALI MASHARTI YA SHULE (FOMU HII IRUDISHWE SHULENI)**

**SEHEMU YA MWANAFUNZI**

1. Mimi ________________________________________ kidato cha ____________ ninakubali kujiunga na Shule ya Sekondari MUUNGANO-1 nikiwa mwanafunzi wa kutwa
2. Ninakubali masharti yote na ninaahidi kufuata sheria zote za Shule.
3. Niko tayari uongozi wa Shule kuchukua hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunirudisha kwa mzazi/mlezi endapo nitakiuka masharti ya Shule

Sahihi ya mwanafunzi ________________________________ Tarehe ______________

**SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi __________ ______________ninakubali mtoto wangu kujiunga na shule ya sekondari MUUNGANO-1 kuanzia tarehe ________________________________-______ Akiwa mwanafunzi wa bweni/kutwa. Ninakubali masharti yote yaliyomo katika maelezo ya kujiunga na shule ikiwa ni pamoja na kutimiza mahitaji mengine ya shule. Nitakuwa tayari kumpokea mtoto wangu wakati wowote endapo atakiuka masharti ya yaliyomo au kubainika kuwa ana afya isiyoridhisha ambayo inahitaji ukaribu na matunzo ya mzazi/mlezi mwenyewe.

(a) Anuani yangu ya kudumu ni

..........................................................................................

..........................................................................................

(b) Jina na anuani ya mlezi wa karibu Tunduma ambaye shule inaweza kuwasiliana naye katika matatizo mbalimbali ya mtoto ni:-

..........................................................................................

..........................................................................................

Sahihi ya mzazi/mlezi ______________________________Tarehe ___________

**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**

## SHULE YA SEKONDARI MUUNGANO-1

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR THE STUDENT**
***(TO BE FILLED IN THE GOVERNMENT HOSPITAL ONLY)***

1. STUDENT'S NAME ...................................................................................................
2. Place Examine the above mentioned student to his fitness for joining advanced level studies in the following tests.
   - (a) Blood Examination Hemoglobin ..............................................................
   - (b) Stool Examination ..........................................................................................
   - (c) Bilharziasis ......................................................................................................
   - (d) Urinalysis ..........................................................................................................
   - (e) Tuberculosis (TB)................................................................................................
   - (f) Eye ...........................................................................................................................
   - (g) Abdomen ..................................................................................................................
   - (h) Asthma ....................................................................................................................
   - (i) Headache ..................................................................................................................
   - (j) Inability to eat some types of food ........................................................................
   - (k) Skin disease ...........................................................................................................
   - (l) Any abnormalities noted above ...............................................................................
   - (m) Any clinic complains ...............................................................................................
   - (n) Any treatment given or recommended ........................................................................
   - (o) Any STD detected ....................................................................................................

**Note: In case of unhealthy detected. It is recommended that a student should get treatment before coming to school.**

I have examined the student above and consider that He/she is physically fit for joining Ordinary level studies.

**Signature of Examiner** ..................................................

**Designation** ........................................................

**Station** ..........................................................

**Rubber stamp** ..................................................

**Date** ..................................................................